**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA UCHUKUZI**

**MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI**

# SEMINA YA KUWAJENGEA UWEZO WANAHABARI (MABALOZI WA LATRA)

**TAREHE 26 - 27 FEBRUARI, 2024, KIBAHA – PWANI**

# MAFANIKO YA LATRA KATIKA KIPINDI CHA MIAKA MITATU YA SERIKALI YA AWAMU YA SITA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Shukrani

Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima, afya njema na fursa nyingine ya kukutana nanyi Wanahabari, Mabalozi wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), ikiwa ni Semina yetu ya kwanza, ili kuwajengea uelewa wa majukumu ya LATRA na pia tuweze kutoa taarifa ya mafanikio ya utendaji wa LATRA katika kipindi cha miaka mitatu (3) ya uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita, chini ya **Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**.

Niwashukuru sana kwa kukubali mwaliko wetu na kuja kuhudhuria kikao hiki cha siku mbili (2) hapa Njuweni Hotel, Kibaha, mkoa wa Pwani. Mahali ambapo wanahabari wapo, Wananchi huwakilishwa vyema. Hivyo ni matarajio yetu kuwa uwepo wenu hapa utawezesha kujifunza na kuufikishia umma wa Watanzania taarifa sahihi kuhusu juhudi kubwa zinazofanywa na Serikali yetu ya Awamu ya Sita inayoongozwa na **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kupitia Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini ili kujenga Taifa bora lenye kuchapa kazi kwa weledi, amani, utulivu, umoja, mshikamano na upendo miongoni mwa Watanzania.

Aidha, nitumie fursa hii kutoa Pongezi za dhati kwa **Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, kwa Uongozi wake Mahiri wenye mafanikio mengi makubwa katika Awamu hii ya Sita. Kwa uchache niseme Uongozi wa Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan umetujengea mazingira mazuri, bora na rafiki ya

kusimamia sekta ya usafiri ardhini kwa weledi na ufanisi mkubwa tukizingatia sana ushirikishwaji wa wadau wetu wote muhimu. Haya yamewezekana kutokana pia na Uongozi mahiri na madhubuti wa wasaidizi wake, wakiwemo Mhe. Prof. Makame Mnyaa Mbarawa (Mb), Waziri wa Uchukuzi, Mhe. David Kihenzile (Mb), Naibu Waziri wa Uchukuzi, Prof. Godius W. Kahyarara, Katibu Mkuu wa Wizara ya Uchukuzi, pamoja na Dkt. Ally Posi, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Uchukuzi.

Aidha, kipekee niwashukuru sana wadau wetu wote, wakiwemo watoa huduma na watumiaji wa huduma za usafiri ardhini. Tunakiri kwamba tumekuwa tukipata ushirikiano mkubwa sana kutoka kwa wamiliki wa vyombo vya moto vinavyofanya kazi kibiashara na tumekuwa tukishirikiana nao katika kutekeleza majukumu yetu ya kiudhibiti. Hawa ni pamoja na watoa huduma mmoja mmoja lakini pia kupitia vyama vyao (mfano: TABOA, TAT, TATOA, TAMSTOA, TFRA, AKIBOA, DARCOBOA, UWADAR na TATO). Tunawashukuru sana kwa ushirikiano na ukaribu wao kwa Mamlaka yetu, na tunaendelea kuwaomba pale wanapokutana na changamoto za kiudhibiti, LATRA ipo tayari kuwasikiliza na kuzitafutia ufumbuzi changamoto zao. Pamoja na hayo, mpango wa Serikali wa kuwashirikisha wananchi katika maamuzi ni hatua muhimu inayosaidia kukabiliana na changamoto mbalimbali kwa njia ya mazungumzo. Jukumu letu la msingi ni kuboresha ustawi wa maisha ya Watanzania kwa kuwasaidia watoa huduma kukuza mitaji yao waliyowekeza, kuimarisha ushindani na kuboresha huduma kwa wananchi.

## 1.2 Kuanzishwa kwa LATRA

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) ilianzishwa kwa Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini Sura 413 ili kudhibiti huduma za usafiri ardhini katika Sekta za Reli, Barabara na Waya. Sheria ya LATRA ilifuta Sheria Na. 9 ya mwaka 2001 iliyoanzisha Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (SUMATRA). LATRA ilianza kutekeleza rasmi majukumu yake tarehe 29 Aprili, 2019 baada ya Sheria yake kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali Namba 358 la tarehe 26 Aprili, 2019.

## 1.3 Uongozi na Wafanyakazi wa LATRA

LATRA inaongozwa na Bodi ya Wakurugenzi yenye wajumbe saba (7) ikiwa ni pamoja na Mwenyekiti wa Bodi (kwa sasa ni Prof. Ahmed Mohamed Ame) ambaye huteuliwa na

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Menejimenti inayoongozwa na Mkurugenzi Mkuu (kwa sasa CPA Habibu J. Suluo) ambaye pia anateuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Muundo wa Mamlaka ina idara tano na vitengo vitano. Kwa sasa, LATRA ina jumla ya wafanyakazi 186 walioajiriwa, ambapo wanaume ni 149 (80%) na wanawake ni 37 (20%). Aidha, tuna wastani wa wafanyakazi 60 kila mwezi ambao wanapata mafunzo ya kazi (internship) kwa maeneo waliyosomea.

### 1.4 Ofisi za LATRA

Mamlaka ina ofisi katika mikoa yote 26 ya Tanzania Bara. Aidha, katika kipindi hiki cha Serikali ya Awamu ya Sita, Mamlaka imeanza kusogeza huduma zake karibu zaidi na wananchi kwa kufungua ofisi katika maeneo ya kimkakati kwenye baadhi ya Halmashari za miji na wilaya hapa nchini, ambapo tayari imefungua ofisi saba (7). Maeneo hayo ni Tegeta-Kibo Complex, Mbagala-Evergreen House na Kituo cha Mabasi cha Magufuli-Mbezi katika Mkoa wa Dar es Salaam. Maeneo mengine ni Makambako-Njombe, Kahama-Shinyanga, Masasi-Mtwara na Ifakara-Morogoro. Taratibu za kufungua Ofisi tatu katika wilaya za Ikwiriri-Pwani, Korogwe-Tanga na Same-Kilimanjaro zinaendelea.

## 2.0 MAJUKUMU NA KAZI ZA MAMLAKA,

Kwa mujibu wa kifungu cha 5 na 6 cha Sheria ya LATRA Sura, 413 kazi na wajibu wa Mamlaka ni kama ifuatavyo:-

### 2.1 Kazi za Mamlaka

Kwa mujibu wa Kifungu cha tano (5) (1) cha Sheria ya LATRA, kazi za Mamlaka ni pamoja na:

a) Kutekeleza majukumu yaliyo chini yake kwa mujibu wa Sheria za kisekta (Sheria ya Leseni za Usafirishaji, 1973 na Sheria ya Reli, 2017 na Sheria ya TAZARA, 1995),
b) Kutoa, kuhuisha na kufuta vibali au leseni za usafirishaji,
c) Kwa kuzingatia Sheria za Kisekta:
    i. Kusimamia viwango vya ubora wa huduma na usalama katika sekta;
    ii. Kusimamia viwango na masharti ya utoaji wa huduma zinazodhibitiwa;

iii. Kudhibiti viwango vya tozo za huduma zinazodhibitiwa.

d) Kuratibu shughuli za usalama wa usafiri ardhini
e) Kusajili wahudumu na kuthibitisha madereva wa sekta zinazodhibitiwa (vyombo vya usafiri wa barabara, reli na waya kibiashara)
f) Kuthibitisha ubora wa vyombo vya usafiri wa reli, ubora wa magari ya abiria na ubora wa magari ya mizigo
g) Kusimamia utendaji wa sekta zinazodhibitiwa ikijumuisha:
    i. viwango vya uwekezaji,
    ii. uwepo wa usalama, ubora na viwango vya huduma,
    iii. gharama za huduma,
    iv. ufanisi wa uzalishaji (uandaaji) na usambazaji (utoaji) wa huduma, na
    v. masuala mengine yanayohusiana na Mamlaka
h) Kuwezesha utatuzi wa malalamiko na migogoro
i) Kutoa taarifa kuhusiana na masuala yanayohusu majukumu ya Mamlaka
j) kushauriana na mamlaka nyingine za udhibiti au vyombo au taasisi zinazotekeleza majukumu sawa na ya Mamlaka Tanzania Bara au mahali pengine popote
k) Kutekeleza majukumu mengine ambayo yamewekwa na Sheria ya LATRA au sheria nyingine za kisekta

### 2.2 Wajibu wa Mamlaka

Kifungu cha sita (6) cha Sheria ya LATRA Sura 413 kinaeleza kuwa kutekeleza majukumu yake, Mamlaka itahakikisha kuwa inakuza ustawi wa jamii ya watanzania kwa:

a) kukuza ushindani na ufanisi wa kiuchumi katika kutoa huduma za usafiri ardhini
b) kuimarisha usalama wa huduma za sekta zinazodhibitiwa ikijumuisha usalama wa watumiaji wa huduma za sekta zinazodhibitiwa
c) kulinda maslahi ya watumiaji kwenye gharama, ubora na viwango vya huduma za usafiri ardhini
d) kulinda uwekezaji wa watoa huduma wenye ufanisi
e) Kuhakikisha huduma zinapatikana na kufikiwa na watumiaji wote wakiwemo watu wenye vipato vidogo, wakazi wa vijijini na watu wenye mahitaji maalum

f) kuelimisha umma kuhusu sekta zinazodhibitiwa, kazi na wajibu wa Mamlaka, haki na wajibu wa watumiaji, uwasilishaji wa malalamiko, migogoro na utatuzi wake,

g) kutunza na kulinda mazingira.

## 2.3 Dira, Dhamira na Misingi Mikuu

Katika jitihada za kutekeleza kazi na majukumu yake, Mamlaka inayo Dira, Dhamira na Misingi Mikuu ambayo huongoza utendaji na utoaji huduma kwa wananchi kila siku kama ifuatavyo:-.

***2.3.1 Dira:*** Nchi yenye huduma za Usafiri Ardhini zilizo salama, za uhakika na rafiki kwa mazingira

***2.3.2 Dhamira:*** Kusimamia huduma za Usafiri Ardhini kwa kutoa leseni, kuzifuatilia na kukuza ushindani kwa ajili ya ustawi wa Watanzania

### 2.3.3 Misingi Mikuu

a) **Uweledi:** Tunaonesha maarifa, ujuzi na mtazamo chanya kwenye kazi zetu

b) **Uwajibikaji:** Tunajitahidi kuwajibika kwa matendo yetu;

c) **Kufanya kazi kwa pamoja:** Tunafanya kazi kwa pamoja ili kufikia malengo yetu tuliyojiwekea;

d) **Uadilifu:** Tuna uaminifu na uadilifu katika kuwahudumia wadau wetu;

e) **Uwazi:** Tunatekeleza majukumu yetu kwa uwazi na kwa ushirikiano; na

f) **Ubunifu:** Tunajitahidi kutafuta njia bora za kuongeza thamani ya huduma zetu

## 3.0 MAFANIKIO YA LATRA KATIKA SERIKALI YA AWAMU YA SITA

Mafanikio ya LATRA katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita chini ya **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,** kwa kipindi cha miaka mitatu (3) kuanzia mwaka wa fedha 2020/21 hadi 2022/23 ni kama ifuatavyo:-

## 3.1 Udhibiti Usafiri wa Barabara


### 3.1.1 Utoaji wa Leseni kwa Vyombo vya Usafiri Kibiashara

**Ndugu Wanahabari,** Kwa mujibu wa Kifungu cha 5(1)( b) cha Sheria ya LATRA, Mamlaka inao wajibu wa kutoa, kuhuisha, kusitisha na kufuta leseni za usafirishaji, hivyo Mamlaka hutoa leseni kila mwaka kwa vyombo vya usafiri kibiashara. Leseni hizi hutolewa baada ya mtoa huduma kukidhi masharti yanayotakiwa kwa aina ya huduma husika. Leseni hizo hutumika kutambua idadi ya watoa huduma wanaodhibitiwa. Katika kipindi cha mwaka **2020/21 hadi 2022/23**, idadi ya leseni za usafirishaji zilizotolewa kila mwaka ziliongezeka kutoka **230,253** hadi **284,158** sawa na ongezeko la leseni **53,905** ambayo ni ongezeko la asilimia **23.4.** Aidha, ukilinganishwa na Mpango wa Mwaka 2022/23 LATRA ilipata mafanikio makubwa ya kuvuka malengo kwenye utoaji wa leseni za usafirishaji wa abiria na mizigo kama inavyooneshwa kwenye Jedwali Na. 1 na Kielelezo Na. 1 hapa chini.

*Jedwali Na. 1: Idadi ya Leseni za Usafirishaji 2020/21 hadi 2022/23*

| SN | Makundi ya Leseni | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mabasi (PSV) | 49,280 | 47,547 | 50,221 |
| 2 | Magari ya Mizigo (GCV) | 141,633 | 143,011 | 169,942 |
| 3 | Pikipiki za magurudumu Mawili | 18,408 | 23,151 | 31,937 |
| 4 | Pikipiki za magurudumu Matatu | 19,698 | 20,577 | 25,512 |
| 5 | Teksi za Kawaida | 291 | 2,654 | 2,305 |
| 6 | Teksi Mtandao | 943 | 3,013 | 3,523 |
| 7 | Mabasi ya kukodi (Special Hire) | | | 718 |
| | **Jumla** | **230,253** | **239,953** | **284,158** |
| | **Ongezeko kwa Mwaka (Idadi)** | **9,182** | **9,700** | **44,205** |
| | **Ongezeko kwa Mwaka (%)** | *4.15%* | *4.21%* | *18.42%* |

*Chanzo LATRA*




*Chanzo LATRA*

Katika mwaka wa fedha 2022/23, Mamlaka ilitoa jumla ya leseni 50,221 za magari ya usafiri wa umma (PSV), ambapo zilifikia asilimia 99.8 ya lengo la leseni 50,290. Jumla ya Leseni za magari ya mizigo 169,942 zilitolewa katika mwaka 2022/23, ambapo zilivuka lengo kwa asilimia 18.8. Hata hivyo katika baadhi ya huduma za usafiri kama pikipiki za magurudumu mawili, pikipiki za magurudumu matatu na teksi kulikuwa na changamoto za mwitikio mdogo wa watoa huduma na hivyo kushindwa kufikia malengo.

Kufuatia changamoto za ukataji wa leseni za magari ya kukodi, hususan pikipiki, katika mwaka wa fedha 2023/24, LATRA imeweka mikakati mipya ikiwa ni pamoja na marekebisho ya Kanuni ya Magari ya Kukodi ya Mwaka 2020 kwa kuruhusu mawakala (authorize agents) ikiwa ni watu binafsi, makampuni, taasisi za umma na vyama vya ushirika kukat a leseni za usafiri wa kukodi na kulipwa kamisheni ya asilimia 20 ya mapato ya ada watakazokusanya.

Kwa sasa LATRA imesaini Hati ya Makubaliano (MoU) na Halmashauri (LGAs) 120 kati ya 185 Nchini kwa lengo la kukasimu LGAs jukumu la kutoa leseni za pikipiki (*Bajaji* na *Bodaboda*) kwa niaba ya LATRA. Katika kipindi cha miaka mitatu (3), LATRA ilirejesha

jumla ya **Shilingi 1,214,921,000** kwa LGAs (**2020/21-Shilingi 297,404,000; na 2021/22-Shilingi 411,513,000, na 2022/23-Shilingi 506,004,000**).

### 3.1.2 Uboreshaji wa Usafiri wa Mijini

Mamlaka imeendelea kuboresha usafiri wa umma katika miji na majiji makubwa hapa nchini. Katika jitihada za kulifungua jiji la Dar es Salaam na maeneo mengine Tanzania Bara, LATRA imeanzisha njia mpya za daladala ili kufika maeneo yasiyofikika na kurefusha baadhi ya njia kwa lengo la kumpunguzia gharama mwananchi kama ifuatavyo:

**a) Dar es Salaam:**

Mkoa wa Dar es salaam njia mpya na ndefu zilizoanzishwa ni pamoja na kutoka:

i. Kivukoni kwenda Bunju Sokoni kupitia Barabara ya Bagamoyo,
ii. Gerezani kwenda Bunju Sokoni kupitia Barabara ya Bagamoyo,
iii. Buyuni Sokoni kwenda Stendi Kuu ya Magufuli kupitia Kinyerezi
iv. Bunju Sokoni kwenda Stendi Kuu ya Magufuli kupitia Madale
v. Mbande Kisewe Kwenda Gerezani kupitia Barabara ya Kilungule, Chang’ombe, Usalama,
vi. Mvuti kwenda Machinga Complex na Tabata Segerea,
vii. Ngobedi B kwenda Machinga Complex kupitia Nyota Njema, na
viii. Kitonga kwenda Gerezani kupitia barabara ya Kilwa.

Aidha, Jijini Arusha, LATRA ilifanya mabadiliko ya njia za daladala kwa kuzifanya baadhi ya njia kuwa za mzunguko kwa lengo kupanua upatikanaji wa huduma kwenye baadhi ya maeneo ya Jiji ambayo hayakuwa na huduma. Mfano wa njia hizo ni kuanzia kwa Mrombo kupitia Impala, Philips, Sanawari, Chuo cha Ufundi Arusha hadi ‘Fire’ na kurudi kwa Mrombo.

**b) Dodoma**

Katika Jiji la Dodoma ambalo ni Makao Makuu ya nchi, zimeanzishwa njia mpya kwa ajili ya kuyafikia maeneo mapya ya makazi mapya kutokana na kukua kwa kasi kwa Jiji la Dodoma. Mfano wa njia hizo ni kutoka:

i) Machinga Complex kwenda Chidachi,
ii) Machinga Complex kwenda Nzuguni, na

iii) Machinga Complex kwenda Swaswa.

Hatua ya kuhamishia daladala kituo cha Machinga Complex kumesaidia kuwepo kwa njia za mzunguko katikati ya Jiji la Dodoma na hivyo kuongeza upatikanaji wa huduma kwa wananchi. Mfano wa mzunguko huo ni kuanzia barabara ya Hospitali kupitia Majengo Sokoni hadi Machinga Complex kisha kupitia Uwanja wa Ndege na kurudi mjini.

### 3.1.3 Uthibitishaji wa Madereva na Usajili wa Wahudumu

**a) Uthibitishaji wa Madereva**

Kwa mujibu wa Kifungu cha 5(1)(e) cha Sheria ya LATRA Sura 413, Mamlaka ina jukumu la kusajili wahudumu na kuthibitisha madereva wa vyombo vinavyodhibitiwa. Lengo la kuthibitisha madereva ni kupata maderea wenye sifa na weledi wa kuendesha magari yanayotoa huduma kwa usafiri wa umma na mizigo kwa kupima umahiri wao ili kuimarisha usalama. Katika hatua ya kutimiza jukumu hilo la Kisheria, Mamlaka imekuwa ikiwasajili madereva na baadae kuwafanyia ithibati. Hadi kufikia tarehe 31 Disemba, 2023, zaidi ya **madereva 21,247** wamesajiliwa na kuingiza taarifa zao kwenye kanzidata ya Mamlaka. Miongoni mwa madereva hawa, **madereva 2,161 wamefaulu** mitihani ya kuthibitishwa na LATRA na kati yao **madereva 1,021 wamesajiliwa** kwenye mfumo wa kufuatilia mwenendo wa mabasi (VTS) na kupatiwa kitufe maalumu cha utambulisho (i-button). Matumizi ya kitufe hicho ni kurahisisha utambuzi wa dereva anayeendesha gari kwa wakati husika kupitia mfumo VTS.

**b) Usajili wa Wahudumu**

Kwa mujibu wa Kifungu cha 5(1)(e) cha Sheria ya LATRA Sura 413 Mamlaka ina jukumu la kusajili wahudumu wa vyombo vinavyotoa usafiri wa umma hapa nchini. Hivyo, LATRA kwa kushirikiana na taasisi nyingine kama vile Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) na Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE); tarehe 1 Julai, 2023 ilifanya uzinduzi wa Mtaala ambao unatumika kufundishia wahudumu wa vyombo vinavyodhibitiwa. Mafunzo kwa wahudumu yalianza tarehe 22 Novemba, 2023. Lengo la mafunzo haya ni kuhakikisha kuwa wahudumu wa vyombo vinavyodhibitiwa wanafahamu Sheria, Kanuni na Taratibu za usafiri ardhini pamoja na kupata uelewa wa namna bora ya kuwahudumia wateja wao pindi wanapokuwa kwenye majukumu yao. LATRA, inapenda kuona wahudumu hawa

wanakuwa nadhifu, wanaheshimu na kuheshimika kwa kazi wanayoifanya pamoja na kuwajengea uwezo wa kutoa huduma bora kwa abiria.

### 3.1.4 Kurejesha Ratiba za Mabasi Kusafiri Usiku (24/7)

Serikali iliamua kuondoa zuio lililowekwa miaka ya 1990 la mabasi ya abiria kusafiri nyakati za usiku. Akitoa uamuzi huo wa Serikali tarehe 28 Juni, 2023 wakati akitoa Hoja ya Kuahirisha Mkutano wa 11 wa Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Tanzania, aliziagiza, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Wizara ya Uchukuzi kuweka utaratibu utakaofuatwa na wamiliki na madereva wa mabasi ya abiria wenye nia ya kusafirisha abiria nyakati za usiku.

LATRA ilishiriki katika maandalizi ya kuruhusu mabasi kusafiri usiku baada ya Tamko la Serikali ambapo safari za usiku zilianza rasmi kuanzia tarehe 1 Oktoba, 2023 baada ta kutolewa kwa Taarifa kwa Umma tarehe 29 Septemba, 2023 na **Mhe. Jumanne A. Sagini (Mb), Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Usalama Barabarani**. Safari hizi zilianza baada ya kukamilika kwa maandalizi ambapo tathmini ya Wizara ya Uchukuzi na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ilionesha kwamba:

a) Udhibiti wa usalama kupitia Jeshi la Polisi umeimarishwa kutokana na jitihada za Serikali ya **Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**.
b) Mwamko wa wananchi, hususan wafanya biashara kutumia taasisi za kifedha badala ya kusafiri na fedha taslimu (cash) umeongezeka.
c) Serikali imeimarisha huduma za mawasiliano ya simu kwa kujenga minara ya mawasiliano kwenye maoneo mengi Nchini.
d) LATRA inao Mfumo madhubuti wa Kufuatilia Mwenendo wa Mabasi (VTS) pamoja na **Kituo cha Huduma kwa Wateja** inaofanyakazi wakati wote (24/7).
e) Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi imeboresha miundombinu ya usafiri, hususan barabara kuu na barabara za mikoa na hivyo kufanya Nchi yetu kuwa moja ya Nchi zenye usafiri wa barabara unaoaminika na bora.

f) Wafanyabiashara wengi wanaomiliki mabasi ya abiria walio tayari kufanya safari za usiku wako tayari pia kuzingatia Sheria, Kanuni na Miongozo kuhusu usafiri na usafirishaji wa abiria.

Kwa ujumla, kumekuwa na mwitikio mkubwa sana kwa wamiliki wa usafiri wa mabasi kwa saa 24 unaungwa mkono na abiria wengi na inaboresha na kukuza shughuli za kijamii na iuchumi.

### 3.2 Udhibiti Usafiri wa Reli

Usafirishaji kwa njia ya reli nchini ni mojawapo ya eneo linaodhibitiwa na LATRA. Mamlaka imeendelea kusimamia usafiri wa reli na kuhakikisha huduma bora na salama zinatolewa na kuhakikisha kuna usalama wa abiria na mizigo. Katika hatua ya kutimiza jukumu hili, LATRA imefanya kaguzi mbalimbali katika miundombunu ya reli za Shirika la Reli Tanzania (TRC) na Mamlaka ya Reli Tanzania na Zambia (TAZARA).

Vilevile, Mamlaka, imeendelea kutoa semina kila mwaka kwa Wafanyakazi Muhimu wa Usalama katika undeshaji wa reli (Safety Critical Workers) kwa TAZARA na TRC ili kuwaongezea ujuzi wa kutimiza majukumu yao kwa weledi. Mafunzo ya aina hii husaidia kuwajengea uwezo wafanyakazi hao muhimu kuzuia ajali zitokanazo na makosa ya kibinadamu (Human Errors). Tathmini inaonesha kwamba, makosa ya kibinadamu katika uendeshaji wa shughuli za reli huchangia zaidi ya asilimia ya 85% ya ajali zote za treni kwa TRC na TAZARA. Hivyo, mafunzo hayo yanalenga kusaidia kupunguza ajali zinazosababishwa na makosa ya kibinadamu.

Katika mwaka wa fedha 2023/2024 Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini imepanga kuhakikisha usalama wa abiria na mizigo unazingatiwa katika usafiri wa reli. Hivyo, Mamlaka itaendelea kufanya kaguzi mbalimbali kwenye miundombinu ya reli za Shirika la Reli Tanzania (TRC) na Mamlaka ya Reli Tanzania na Zambia (TAZARA) ili kubaini mapungufu yanayoweza kuhatarisha usalama wa treni. Kaguzi hizi huainisha vihatarishi vyote na kutengeneza mpango mkakati wa kurekebisha kwa lengo la kuzuia matukio ya ajali. Maeneo yanayoangaliwa ni pamoja na madaraja, reli, mifereji ya maji, vifungashio

vya reli na ushindiliaji wa kokoto kwenye tuta la reli na maungio. Hili ni jukumu la msingi kwa Mamlaka ili kuhakikisha ~~ubora na~~ usalama wa usafiri wa reli hapa nchini.

Kwa upande wa SGR, Mamlaka inaendelea na ukaguzi wa miundombinu inayoendelea kujengwa ili kuhakikisha kuwa ni salama. Aidha Mamlaka itafanya ukaguzi wa vichwa, mabehewa na miundombinu ya SGR kabla havijaanza kutumika.

### 3.3 Udhibiti Usafiri wa Waya (Cable Transport Regulation)

Usafiri wa Waya ni moja kati ya aina za usafiri mijini na maeneo yenye milima au kwenye vivuko. Katika kudhibiti usafiri wa waya Nchini. Usafiri huu ulianzia Colombia mwaka 2004 kama aina mojawapo ya usafiri wa mjini (metrocable cars) na kwa sasa umeenea sehemu nyingi duniani na pia ni kivutio pcha utalii.

Utafiti wa awali umeonesha kuwepo fursa za uwezekano wa kuwekeza usafiri huu kitalii hapa Nchini, ili kuunga mkono juhudi za Mhe. Rais za Royal Tour. Maeneo yenye fursa hiyo ni Arusha, Kilimanjaro, Mbeya, Iringa, Morogoro, Tanga na Dar es Salaam.

LATRA inapaswa kisheria kudhibiti usafairi huu na kwa kuwa haikuwa katika Muundo wa Taasisi wakati LATRA ilipoanza kutekeleza majukumu yake mwaka 2019, Bodi ya Wakurugenzi imefanyia mapitio Muundo wa Uongozi na kuwasilisha mapendekezo Serikalini ili kuwe na Kitengo cha Udhibiti Usafiri wa Waya. Aidha, LATRA imeshaandaa rasimu ya Kanuni ya Udhibiti wa Usafiri wa Waya ili kupendekeza mchakato wake Wizara ya Uchukuzi na kwa kuwa jambo hili ni jipya hapa Nchini, Bodi ilielekeza atafutwe Mshauri wa Kimataifa (International Consultant) ili aipitie rasimu ya Kanuni na kuishauri vyema LATRA. Mchakato wa kumpata mshauri mwelekezi unaendelea.

### 3.4 Kukuza matumizi ya TEHAMA kwenye utoaji wa huduma

#### 3.4.1 Mfumo wa Usimamizi wa Shughuli za Kiudhibiti (RRIMS)

Mamlaka imejenga mfumo wa TEHAMA unaojulikana kama Railway and Road Information Managemet System (RRIMS). Mfumo huu unatumika kwa ajili ya maombi ya leseni za usafirishaji pamoja na kazi zingine za usimamizi wa shughuli za kiudhibiti za Mamlaka. Mfumo huu umeunganishwa na mifumo ya taasisi nyingine za serikali kama

vile TRA, TIRA, NIDA, GePG na BRELA. Halikadhalika, RRIMS imeunganishwa na mifumo ya wadau wengine kama vile watoa huduma wa tiketi mtandao. Lengo la kuunganisha mfumo huu na mifumo mingine ni kurahisisha utoaji huduma za Mamlaka kwa wananchi.

Mfumo wa RRIMS hutumika kutoa leseni za usafirishaji na unamwezesha mteja kufanya maombi kutokea mahali popote alipo. Maombi yote yanayowasilishwa yanafanyiwa kazi siku hiyo hiyo na kuhakikisha mwananchi anapata leseni chini ya saa 24. Aidha, Mamlaka inaendelea kuboresha mfumo huu ili kuanza kutoa leseni za kielektroni na hivyo kuondoa hitaji la wateja kutembelea ofisi za Mamlaka kwa ajili ya kufuata leseni. Maboresho hayo yatakapokamilika yatasaidia kuongeza ufanisi na kupunguza kwa kiwango kikubwa muda wa kupata huduma za leseni.

### 3.4.2 Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS)

Kwa mujibu wa Kifungu cha 5(1)(d) na Kifungu cha 6(g) cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini, Sura ya 413, Mamlaka ina jukumu la kuratibu usalama wa vyombo vinavyodhibitiwa pamoja na kuhifadhi mazingira. Hivyo, Mamlaka ilianzisha Mfumo wa kufuatilia mwenendo wa Magari (Vehicle Tracking System – VTS) ambao ni mfumo wa kielectroni unaohusisha ‘Satelite’, Kifaa cha Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTD), Mtandao wa Mawasiliano na Vifaa vya Uhifadhi Data Taarifa (GPS Data Servers) vinavyofanya kazi kwa pamoja ili kutuma taarifa za mwenendo mzima wa safari za chombo husika.

Mfumo wa VTS ulianza kutumika rasmi mwaka 2017 chini ya SUMATRA na baada ya kufutwa kwa Sheria ya SUMATRA mwaka 2019, mfumo huu ulirithiwa na LATRA. Tangu kuanzishwa kwa mfumo wa VTS, Mamlaka imefanikiwa katika mambo mengi ikiwemo:

a) Kuunganisha jumla ya magari **10,110** yameunganishwa kwenye mfumo huu ambapo, magari **7,920** yanaonekana yakiendelea kutoa taarifa (yapo hai) – **2,190** hazionekani - na kwa leo saa 2:45 asubuhi , magari **4,724** yanatuma taarifa;
b) Kupunguza kwa kiasi kikubwa ajali za barabarani zinazotokana na mwendokasi;
c) Kupunguza madhara ya ajali zinazotokana na mwendokasi;
d) Kurahisisha uchunguzi wa ajali pale zinapotokea; na

e) Kumtambua dereva anayeendesha gari kupitia kitufe cha utambuzi *(i-button)* ambacho kinaunganishwa moja kwa moja na mfumo wa VTS.

Aidha, kutokana na faida za mfumo huu, Serikali kupitia LATRA imefanikiwa kuimarisha usalama na hivyo kuboresha utoaji huduma za mabasi kwa kuruhusu huduma ya usafiri huo kwa masaa 24. Hatua hii imesaidia wananchi kufanya shughuli zao za kiuchumi kwa ufanisi zaidi kwa kuwa wanaweza kusafiri muda wowote na hivyo kuongeza uzalishaji.

#### 3.4.3 Huduma wa Tiketi Mtandao

Mabasi yote ya masafa marefu yameunganishwa na mfumo wa Tiketi Mtandao na kwa kiasi kikubwa mfumo umesaidia kudhibiti upandishaji holela wa nauli. Mamlaka imeandaa Kanuni mahususi kwa ajili ya kusimamia eneo hili ikiwa ni pamoja na kuweka masharti kwa watoa huduma wa mifumo ya Tiketi Mtandao.

#### 3.4.4 Huduma za Teksi/Pikipiki Mtandao (Ride hailing)

Huduma ya usafiri wa kukodi kwa njia ya mtandao imeendelea kukua kwa kasi kubwa tangu ilipoanza hapa nchini mwaka 2017. Hadi kufikia tarehe 27 Februari, 2024, jumla ya Kampuni 20 zenye mifumo ya kutoa huduma ya teksi/pikipiki mtandao (ride hailing platform operator) zilikuwa zimewasilisha maombi ya Leseni LATRA na yalikidhi mahitaji ya kisheria ambapo kampuni 19 zimeshalipia ada za leseni na kupatiwa leseni hizo, na kampuni moja, **Teksol Limited (Rova Ride)**, haijalipa ada na hivyo haikupewa leseni. Hivyo, kampuni 19 zilizopatiwa leseni ni **Proin, Bolt, Little Ride, Globcab, Tanzania App System, Nikar, Twende, Faras, Zanzicab, Tirhal, Interactive Tours, Chapu Ride, Uber, ChapRide, Tanswift, Quickii, Smart Driver, Boda Official** na **Nipitie.**

Aidha, kuna kampuni nne (4) ambazo zilikamilisha mchakato wote mpaka kuunganisha mifumo yao na LATRA **ili tuweze kuona na kufuatilia magari yao na nauli zinazolipwa**, lakini hawajarudi kuomba leseni na hatujui wanatoa huduma kimya kimya au wako wapi. Kampuni hizo ni **Suka Ride, Moovn, Viso Ride na Akili Ride.**

Hivyo, ili kampuni hizi zitoe huduma, wateja wao ni teksi/pikipiki mtandao. Leseni ambazo zimetolewa kwa teksi/pikipiki mtandao hadi sasa ni **13,721** lakini leseni hizi

huwa na uhai wa mwaka mmoja. Idad ya leseni zilizotolewa kila mwaka ni **2021/22 – leseni 3,144; 2022/23 - leseni 3,598 na 2023/24 - leseni 6,979).**

Kwa hiyo, huduma hii ina udhibiti wa makundi matatu: mmiliki wa mfumo ya teksi/pikipiki mtandao, mmiliki (dereva) wa gari, na abiri (nauli). Hivyo, tunapopanga nauli za huduma hii, tunaweka kiwango cha chini (kisishuke) ili kumlinda mmiliki (dereva) na kiwango cha juu (kisizidi) kumlinda abiria. Mmiliki wa mfumo ya teksi/pikipiki mtandao yeye anapata kamisheni ya nauli, nayo kuna kima cha chini na cha juu) ambacho kinatoa uhuru kwa wamiliki (madereva) kumchagua mwenye nafuu na maslahi kwake.

### 3.4.5 Mfumo Tumizi wa LATRA (LATRA App)

Mamlaka imeandaa mfumo tumizi wa LATRA unaopatikana ‘Play Store’ kwenye simu zote za Android. Huduma hii inamwezesha mwananchi kupata taarifa za nauli za mabasi ya masafa marefu na mabasi ya mijini. Kwa sasa Mamlaka inaendelea kuboresha huduma za mfumo huo ili kuwezesha abiria kutambua mwendo kasi wa gari.

### 3.4.6 Matumizi ya Mfumo wa e-Mrejesho

Mamlaka iimejiunga na Mfumo wa Serikali wa e-Mrejesho unaotumika kwa ajili ya kupokea Malalamiko, Mapendekezo, Pongezi au Maulizo. Mfumo unapatikana kwa anwani ya https://emrejesho.gov.go.t/ au kwa kupakua mfumo tumizi wa e-Mrejesho au kwa kutumia simu kwa njia ya msimbo (USSD) au kwa kupitia tovuti ya Mamlaka https://www.latra.go.tz/ sehemu ya tovuti mashuhuri. Hivyo, tunawasihi wananchi wote kutumia mfumo huo na tunawahakikishia kushughulikia masuala yatakayowasilishwa ndani ya siku 21 tangu utakapowasilisha lalamiko au maulizo yako.

### 3.4.7 Matumizi ya Mfumo wa NeST

Mamlaka imejiunga na inatumia Mfumo wa Taifa wa Ununuzi wa Umma wa Kieletroni (NeST) kwa ajili ya kutangaza na kuchakata zabuni mbalimbali. Nitumie nafasi hii kuwashauri wazabuni wajisajili kwenye mfumo huu ambao unapatikana kwenye tovuti ya Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) ili kuweza kushiriki kwenye zabuni Serikalini.

## 3.5 Elimu kwa Umma na Maonesho


### 3.5.1 Uandaaji na Urushaji wa Vipindi vya Elimu kwa Umma

Mamlaka kupitia studio yake iliyoko Dar es salaam imeendelea kuandaa vipindi na kuvirusha kupitia Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC1) kila siku ya Jumanne saa 3:30 usiku na kwenye mitandao ya kijamii kama vile 'LATRA Online TV' na Instagram ambapo kwa mwaka wa fedha ulioshia Juni, 2023 jumla ya vipindi 115 viliandaliwa na kurushwa. Aidha katika mwaka wa Fedha 2023/24 kuanzia Julai hadi Desemba, 2023 jumla ya vipidi 91 kama hivyo viliandaliwa na kurushwa kupitia TBC 1 na mitandao ya kijamii ili kuelimisha umma kuhusu masuala mbalimbali ya kiudhibiti yanayotekelezwa na LATRA. Vilevile, taarifa za LATRA zinapatikana kwenye tovuti ya Mamlaka kupitia www.latra.go.tz pamoja na mitandao mingine ya kijamii kama vile facebook na twitter. Aidha, LATRA imeendelea kushirikiana na vyombo vingine vya habari kwa kushiriki katika midahalo na vipindi vinavyoandaliwa na vyombo hivyo ili kuwapatia uelewa wananchi wanaofuatilia midahalo na vipindi hivyo.

**Vipindi hivi vilijumuisha Semina ya Wabunge wote wa Bunge la Tanzania iliyofanyika Bungeni Dodoma, tarehe 10 Novemba, 2022 kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi na TIRA. Semina hii ilikuwa na ufanisi mkubwa na ilihudhuriwa pia na Spika na Naibu Spika. Aidha, ilijumuisha ziara za Kamati za Kudumu za Bunge (Hesabu za Serikali, Miundombinu, na Uwekezaji wa Mitaji ya Umma).**

**Jedwali Na. 2: Vipindi vya Televisheni na Mitandao ya Kijamii, 2020/21-2022/23**

| Na. | Aina ya Vipindi | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Vipindi vya Runinga (TV) | 40 | 48 | 52 | **140** |
| 2 | Mitandao ya kijamii | 12 | 30 | 63 | **105** |
| | **Jumla** | **52** | **78** | **115** | **245** |




### 3.5.2 Kushiriki katika maonesho

Aidha, LATRA imeendelea kushiriki kwenye maonesho mbalimbali ya Kitaifa na Kisekta kwa lengo la kutoa elimu kwa wananchi. Katika maonesho ya Sabasaba ya mwaka huu, LATRA ilipata ushindi wa kwanza miongoni mwa mamlaka za udhibiti kutokana na ubora wa maonesho yake. Aidha, LATRA imeshiriki katika maonesho mbalimbali kama Wiki ya Ufuatiliaji na Tathini iliyoandaliwa na Wizara ya Uchukuzi mwezi Septemba, 2023 na Mkutano wa 16 wa Mwaka wa Sekta ya Uchukuzi mwezi Desemba, 2023 Jijini Arusha kwenye Kituo cha Mikutano ya Kimataifa Arusha (AICC).

Katika mwaka huu wa fedha 2023/24, LATRA imepanga ratiba ya kukutana na makundi mbalimbali ya wadau kwa ajili ya kupata mrejesho kutoka kwao kuhusiana na huduma tunazozisimamia.

### 3.5.3 Kuanzisha Kituo cha Huduma kwa Wateja

Katika mwaka wa fedha 2022/23 Mamlaka imeanzisha kituo cha huduma kwa wateja kinachofanya kazi kwa saa 24 na siku zote za wiki (24/7) ili kurahisisha utoaji huduma kwa wateja na kuwezesha utatuzi wa migogoro na changamoto mapema. Huduma za kituo hicho zinapatikana kupitia namba za kupiga bila malipo **0800110019** na

**0800110020**. Aidha mamlaka imeendelea kuzitangaza namba hizi kupitia vipindi vya elimu kwa umma, mitandao ya kijamii na kuzibandika katika maeneo mbalimbali yanayofikiwa na wadau wetu. Aidha, kwa sasa namba hizi zimeanza kuandikwa kwenye milango ya mabasi ya mijini sambamba na viwango vya nauli.

## 3.6 Ushirikishwaji wa Wadau na Utatuzi wa Migogoro

### 3.6.1 Ushirikishwaji wa Wadau

Kwa mujibu wa Kifungu cha 21 cha Sheria ya LATRA, Sura 413 Mamlaka huwashirikisha wadau wakati wa kutekeleza majukumu yake. Hivyo, Mamlaka imeendelea kuwashirikisha wadau pindi inapotekeleza majukumu yake kwa kukusanya maoni yao au kutoa elimu. Ushirikishwaji huu unafanyika kwa njia ya mikutano mbalimbali ya wadau inayolenga kusikiliza kero za wadau kwa lengo la kutafuta ufumbuzi kwa pamoja, kupokea maoni, mapendekezo na ushauri mbalimbali kabla ya kutoa maamuzi. Katika mwaka wa fedha 2022/23 LATRA ilifanya jumla ya mikutano ya wadau 36 ikiwemo mikutano 9 ya kupokea maoni kuhusu mapitio ya nauli, mikutano 6 ya mabadiliko ya kanuni, mikutano 6 ya kutoa elimu kuhusu masuala kuidhibiti, mikutano 7 ya kutunza mazingira na kuimarisha usalama wa usafiri ardhini. Aidha, Mamlaka ilifanya mikutano 8 kwa ajili ya kuzitafutia ufumbuzi kero mbalimbali kwenye usafiri wa barabara na reli.

### 3.6.2 Utatuzi wa Migogoro

Moja ya kazi za Mamlaka kwa mujibu wa Kifungu cha 5(1)(h) cha Sheria ya LATRA Sura ya 413 ni kutatua migogoro inayojitokeza kwenye huduma zinatolewa kwenye sekta zinazodhibitiwa. Kutokana na ukubwa wa sekta, Mamlaka inapokea malalamiko mengi ya wadau hususan watuamiaji wa huduma dhidi ya watoa huduma. Kutokana na mfumo mzuri wa utatuzi wa migogoro uliowekwa na Mamlaka, migogoro ipatayo 234 iliyowasilishwa kwa Mamlaka kwa mwaka wa fedha wa 2022/23 na iliweza kutatuliwa na kuishia kwenye ngazi ya Mamlaka. Aidha, katika mwaka wa Fedha, 2023/24 kuanzia Julai hadi Desemba, 2023 jumla ya malalamiko 119 yalipokelewa ambapo malalamiko 108 sawa na asilimia 90.7 yaliftatuliwa na malalamiko nane (8) yaliyosalia yanaendelea kufanyiwa kazi. Malalamiko mengine matatu (3) yanafanyiwa kazi kupitia Kamati Maalumu ya Mamalaka kwa mujibu kifungi cha 33 cha Sheria ya LATRA, Sura 413.

### 3.7 Ufuatiliaji wa Masharti ya Leseni

Kila mwaka Mamlaka hutenga bajeti kwa ajili ya shughuli za ufuatiliji wa uzingatiajiwa masharti ya leseni. Maafisa wa Mamlaka kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi hufanya kaguzi kwenye maeneo ya mijini na barabara kuu kwa lengo la kuhakikisha huduma za usafirishaji zinatolewa kwa kuzingatia sheria.

## 4.0 MAPATO YA MAMLAKA

**Ndugu Wanahabari,** Vyanzo vya mapato ya Mamlaka vimeainishwa katika Kifungu cha 35 (1) cha Sheria ya LATRA, Sura 413. Sheria hiyo inabainisha vyanzo vya mapato kama ifuatavyo:

i. Mapato yatokanayo na kutoa leseni mpya na kuongeza muda wa leseni zilizoisha;
ii. Mapato ya levi kutoka kwa watoa huduma;
iii. Malipo au mali kwa Mamlaka zitokanazo na shughuli za Mamlaka;
iv. Michango na Misaada inayotolewa kwa Mamlaka;
v. Fedha nyingine zozote zinazopatikana kisheria kutokana na Mamlaka kutekeleza majukumu yake.


Mapato ya Mamlaka yamekuwa yakiongezeka mwaka hadi mwaka. Katika kipindi cha mwaka wa fedha **2020/21 hadi 2021/22**, mapato ya Mamlaka yaliongezeka kutoka **Shilingi Bilioni 25.95** hadi **Shilingi Bilioni 28.53** ikiwa ni ongezeko la **Shilingi Bilioni 2.58** sawa na ongezeko la **10.0%.** Aidha, katika kipindi cha mwaka wa fedha **2021/22 hadi 2022/23**, mapato ya Mamlaka yaliongezeka kutoka **Shilingi Bilioni 28.53** hadi **Shilingi Bilioni 34.25** (kabla ya kukamilika ukaguzi wa CAG) ikiwa ni ongezeko la **Shilingi Bilioni 5.72,** sawa na ongezeko la **20.1%**.

Kwa jumla, katika kipindi cha miaka mitatu (3) ya utekelezaji wa majukumu ya LATRA, mwaka wa fedha **2020/21 hadi 2022/23**, mapato ya Mamlaka yaliongezeka kutoka **Shilingi Bilioni 25.95** hadi **Shilingi Bilioni 34.25** (kabla ya kukaguliwa na CAG) ikiwa ni ongezeko **la Shilingi Bilioni 8.31** sawa na ongezeko la **32%** kama inavyooneshwa kwenye Jedwali Na. 3 na Kielelezo Na. 3 hapa chini..

***Jedwali Na 3: Mapato ya Mamlaka kwa Mwaka 2020/21-2022/23 (Sh. '000')***

| Na. | Makundi ya Mapato | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | Ongezeko | % |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Ada ya Leseni | 16,648,057 | 17,082,484 | 19,269,429 | **2,621,372** | **16%** |
| 2 | Levi za Watoa Huduma | 454,219 | 479,941 | 1,177,586 | **723,367** | **159%** |
| 3 | Mapato Mengineyo | 8,843,227 | 10,966,529 | 13,803,854 | **4,960,627** | **56%** |
| **Jumla** | | **25,945,503** | **28,528,954** | **34,250,869** | **8,305,366** | **32%** |

*Chanzo: LATRA*




*Chanzo: LATRA*


## 5.0 KUCHANGIA MFUKO MKUU WA SERIKALI NA TAASISI NYINGINE

Mamlaka hupaswa kuchangia asilimia 15 ya mapato yake ghafi kwenda kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali (Consolidated Fund) kwa mujibu wa Kifungu cha 11(3) cha Sheria ya Fedha za Umma, Sura ya 348 (Public Finance Act, Cap. 348). Aidha, Mamlaka hutakiwa kuchangia asilimia 70 ya fedha za ziada (surplus funds) kila mwisho wa mwaka wa fedha kwenda katika Mfuko Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa kifungu cha 42 cha Sheria ya Bajeti, Sura ya 439. Katika kipindi cha miaka mitatu (3), kuanzia Mwaka wa fedha **2020/21 - 2022/23**, Mamlaka imeweza kuchangia **Shilingi Bilioni 12.81** katika Mfuko Mkuu wa Serikali, kama inavyooneshwa kwenye Jedwali Na. 4 na Kielelezo Na. 4.

***Jedwali Na. 4: Michango Kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali - 2019/20 hadi 2022/23***

| Na. | Mwaka | Mchango wa 15% (Sh.) | Mtaji wa ziada (Excess Capital) (Sh.) | Jumla (Sh.) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 2020/21 | 3,817,959,600 | 1,000,393,400 | 4,818,353,000 |
| 2 | 2021/22 | 4,279,343,100 | 404,395,900 | 4,683,739,000 |
| 3 | 2022/23 | 4,711,279,346 | 0 | 4,711,279,346 |
| **Jumla** | | **12,808,582,046** | **1,404,789,300** | **14,213,371,346** |

*Chanzo: LATRA*




*Chanzo: LATRA*

Pamoja na hayo, Mamlaka imeweza kuchangia taasisi mbalimbali za kitaifa na kimataifa kwa niaba ya Serikali ikiwa ni sehemu ya matumizi yake. Taasisi hizo ni pamoja na Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Usafiri Ardhini (LATRA CCC, Tume ya Ushindani (FCC), Baraza la Ushindani Tanzania (FCT), Jukwaa la Afrika la Wadhibiti wa Huduma (African Forum for Utilities Regulators - AFUR) na Umoja wa Taasisi za Reli Kusini mwa Afrika (Southern Africa Railways Association, SARA).

Mamlaka hupaswa kuchangia asilimia 15 ya mapato yake ghafi kwenda kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali (Consolidated Fund) kwa mujibu wa Kifungu cha 11(3) cha Sheria ya

Fedha za Umma, Sura ya 348 (Public Finance Act, Cap. 348). Aidha, Mamlaka hutakiwa kuchangia asilimia 70 ya fedha za ziada (surplus funds) kila mwisho wa mwaka wa fedha kwenda katika Mfuko Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa kifungu cha 42 cha Sheria ya Bajeti, Sura ya 439.

Katika kipindi cha miaka mitatu (3), mwaka wa fedha **2020/21** - **2022/23**, Mamlaka imeweza kuchangia **Shilingi Bilioni 14.21** katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

## 6.0 UKAGUZI WA HESABU ZA MAMLAKA

### 6.1 Mamlaka y Kukagua Hesabu za LATRA

Kwa mujibu wa kifungu cha 143 cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama ilivyofafanuliwa na kifungu cha 9 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma (the Public Audit Act (PAA) No 11 of 2008), CAG ndiyo mwenye mamlaka ya kukagua Hesabu za TASAC. Hata hivyo, kwa mamlaka aliyonayo CAG yaliyoelezwa katika kifungu cha 33(1) cha Sheria hiyo, anaweza kuteua kampuni nyingine kufanya ukaguzi kwa niaba yake au kwa kushirikiana na CAG. Katika mwaka wa fedha **2020/21-2022/23**, CAG alifanya ukaguzi wa Hesabu za LATRA kwa kushirikiana na Kampuni ya Ukaguzi ya Auditax International ya Dar es Salaam (2020/21-2021/22) na Kampuni ya Dar es Salaam Financial Consultants (2022/23).

### 6.2 Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

Katika kipindi cha miaka yote mfululizo tangu kuanzishwa kwa Mamlaka, LATRA ilifanikiwa kupata **HATI SAFI (Clean Audit Report/ Unqualified Audit Opinion)** kutoka kwa CAG (tunasubiri matokeo ya 2022/23) na aliridhika kwamba Hesabu za LATRA ziliandaliwa na kuwasilishwa kwa kuzingatia viwango vya Kimataifa vya kuandaa hesabu kwa taasisi za umma, yaani ***the International Public Sector Accounting Standards (IPSASs)*** pamoja na kuzingatia Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2011 na Kanuni zake za mwaka 2013.

### 6.3 Mashindano ya Ubora wa Kuandaa na Kuwasilisha Hesabu

Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi (NBAA) hualika Taasisi za Umma na Sekta Binafsi kushiriki kila mwaka katika mashindano ya ubora wa kuandaa na kuwasilisha hesabu za zilizokaguliwa na kupata Hati Safi (Unqualified Audit Opinion). Hesabu hizo hufanyiwa tathmini na Kamati ya Wataalamu wa NBAA kwa kuzingatia viwango vya kimataifa vya kuandaa na kuwasilisha hesabu. Mashindano haya hujulikana kama *The Best Presented Finacial Statements Awards*. Lengo ni kuongeza hamasa ya kuzingatia viwango vya kimataifa na kuboresha hesabu za taasisi nchini. NBAA hutoa tuzo kwa washindi katika Mkutano Mkuu wa Mwaka (NBAA Annual Conference) unaofanyika wiki ya kwanza ya mwezi Disemba na pia hutoa mrejesho kwa kila mshiriki kwa kuainisha mapungufu na kuelekeza maeneo ya kuboresha katika Hesabu husika.

Tunapenda kuutaarifu umma kwamba LATRA ilishiriki mashindano hayo kwa mara ya kwanza mwaka 2023 kwa kuwasilisha hesabu zake za mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni, 2022 na kuibuka na Tuzo ya Mshindi wa Pili katika kundi la Taasisi za Udhibiti Nchini linaloandaa hesabu zake kwa viwango vya kimataifa vya IPSASs. LATRA inakusudia kuendelea kushiriki mashindano haya kwa kuwa yanatoa mrejesho wa maeneo ya kuboresha.

## 7.0 HITIMISHO

Kwa mwaka huu wa fedha 2023/2024 LATRA imejipanga kuhakikisha kuwa huduma bora na salama za usafiri ardhini zinawafikia wananchi, kuondoa kero na changamoto mbalimbali katika sekta. Hii ni katika kutekeleza maelekezo anayoyatoa **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** mara kwa mara.

Pia, Mamlaka imejipanga kusimamia huduma za usafiri ardhini ambapo huduma za usafiri wa barabara na reli zina mchango mkubwa katika kukuza uchumi na kuwezesha Tanzania kufanya biashara na Nchi za Jumuia ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na nchi za Jumuia ya Afrika Mashariki (EAC).

Nitumie fursa hii kuwashukuru Wanahabari wote kutoka vyombo mbalimbali vya habari kwa kuendelea kufikisha kwa jamii kile ambacho Mamlaka imekuwa ikikifanya kwa

maslahi ya umma, na kwa ushirikiano ambao mmekuwa mkituonesha kila tunapowahitaji bila kuchoka.

Aidha, naomba kutumia fursa hii kuwakaribisha LATRA Makao Makuu, Dodoma na pia katika ofisi zetu ambazo zipo mikoa yote Tanzania Bara, endapo kuna jambo mnahitaji kutoka kwetu, milango iko wazi karibuni sana na tupo tayari kushirikiana nanyi. Ninyi ni wadau wetu wakubwa na muhimu sana, **tutaendelea kuwashika kwa mikono miwili tukitambua thamani ya kalamu zenu kwetu, kwa Taifa letu na dunia kwa ujumla**.

**Asanteni Sana Kwa Kunisikiliza.**

**MKURUGENZI MKUU- LATRA**